

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



“Mtaa wa Bagara
Miyomboni,
S.L.P. 386,
27103 MANYARA,
Barua Pepe: rbcmanyara@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

MANYARA – AGOSTI 16, 2020

**MWENYEKITI WA KIJJI ASHIKILIWA NA TAKUKURU
KWA RUSHWA YA NGONO**

TAKUKURU Wilaya ya Kiteto Mkoani Manyara inamshikilia Mwenyekiti wa Kijiji cha Kimana Wilson Ngolanya (63) kwa tuhuma za rushwa ya Ngono.

Ngolanya alikamatwa tarehe 15 Agosti, 2020 majira ya jioni katika nyumba ya kulala wageni iitwayo Naisimo iliyoko Mjini Kibaya akiwa uchi wa Mnyama, akiwa amevalia Kondomu tayari kwa kutekeleza uhalifu huo.

Awali tulipokea taarifa toka kwa mlalamikaji binti wa miaka 23 (Jina linahifadhiwa) akimtuhumu Mwenyekiti huyo wa kijiji kwa kuomba rushwa ya ngono.

Kwa mujibu wa uchunguzi Ngolanya alikuwa akiomba rushwa ya ngono ili aweze kumsaidia mlalamikaji kuwaondoa wavamizi watatu (3) kwenye shamba lililoluwa likimilikiwa na baba wa binti huyo ambaye kwa sasa ni marehemu.

Uchunguzi unaonyesha kuwa Ngolanya anafahamu kuwa shamba hilo lilikuwa la marehemu baba wa binti huyo. Hata hivyo alimtaka binti huyo ampe rushwa ya ngono ili aweze kuwaondoa wavamizi hao katika shamba la marehemu baba yake.

Binti huyo baada ya kuona usumbufu unazidi alitoa taarifa TAKUKURU na baada ya kujiridhisha na uchunguzi wa awali, Makachero wetu waliandaa mtego

uliopelekea kukamatwa kwa mtuhumiwa katika moja ya vyumba katika nyumba ya kulala wageni iitwayo Naisimo akiwa tayari amevua nguo zake zote na kuvaa kondomu ili kutimiza uhalifu huo.

Kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007 kinasema; Mtu yeyote aliye kwenye mamlaka au uongozi ambaye kwa kutumia mamlaka au cheo alichonacho akilazimisha sharti la rushwa ya ngono ili aweze kumpa mtu yeyote ajira, kupandishwa cheo, kumpa haki stahiki, upendeleo au unafuu asiostahili anakuwa ametenda kosa la rushwa ya ngono na ikithibitika atastahili adhabu ya fine isoyozidi milioni tano (sh.5,000,000) au kifungu kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

Rai yetu kwa viongozi wachache ndani ya utumishi wa umma na binafsi wenye tabia au fikra kama za Ngolanya za kuomba rushwa ya ngono waache mara moja kwa kuwa sheria ni msumeno hukata mbele na nyuma.

Tuwaombe pia mabinti pale wanapokutana na kudaiwa rushwa ya ngono kinyume na K/F cha 25 PCCA Na. 11/2007 kama kilivyofafanuliwa hapo juu, watoe taarifa TAKUKURU kwa namba yetu ya dharura 113 au ofisi za TAKUKURU Mikoa na Wilaya zilizopo karibu ili kuwaondoa hawa wachache wanaotumia vyeo walivyonavyo kudhalilisha utu kwa kulazimisha rushwa ya ngono.

Imetolewa na:

**HOLLE MAKUNGU
MKUU WA TAKUKURU (M)
MANYARA**